MWONGOZO WA MAJUKUMU YA KUTEKELEZA NA KURIPOTI UNAOHUSU VIKWAZO VYA UMOJA WA MATAIFA VILIVYOWEKEWA JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA WATU WA KOREA

Imetayarishwa na Mark Duncan

1. Muhtasari wa Utendaji

- Mfumo wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa unaolenga Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea ni mfumo mkali zaidi uliopo, unaolazimu serikali zitekeleze mkusanyiko tata wa majukumu ya kutekeleza kisheria na kuripoti;
- Mataifa barani Afrika yanaweza kuathirika kwa urahisi na ukwepaji vikwazo kwa ajili ya uhusiano wao wa kibiashara wa muda mrefu na Korea Kaskazini uliokuwepo kabla ya kuidhinishwa kwa mfumo wa vikwazo lakini ambao huenda ukawa si halali kisheria baada ya 2006, unarahisisha ukwepaji unaofanywa na Korea Kaskazini, raia na mashirika yake;[1]
- Ili kurahisisha utiifu, mwongozo huu unatoa muhtasari wa aina za hatua za vikwazo zilizowekewa Korea Kaskazini, juhudi za utekelezaji kisheria na majukumu ya kuripoti.

Mfumo wa Vikwazo Vilivyowekewa Korea Kaskazini

Mfumo wa Vikwazo Vilivyowekewa Korea Kaskazini (hapa ndani baadaye “mfumo wa 1718”) uliidhinishwa na azimio la Baraza la Usalama la 1718 (2006),[2] ambalo pia lilianzisha kamati husika ya vikwazo (hapa ndani baadaye “Kamati ya 1718”), na ulipanuliwa na maazimio ya Baraza la Usalama ya 1874 (2009), 2087 (2013), 2094 (2013), 2270 (2016), 2321 (2016), 2371 (2017), 2375 (2017) na 2397 (2017). [3]

[1] *Mwongozo wa Utekelezaji wa Vikwazo vya Umoja wa Mataifa vilivyowekewa Korea Kaskazini: Changamoto Zinazokumba Mataifa barani Afrika*, Shirika la Kimataifa la Utiifu na Uwezo & Taasisi ya Umma ya Utafiti & Maendeleo ya Marekani, Januari 2019 [ukurasa 9-26]

[2] *Azimio la Baraza la Usalama la 1716 (2006)*, Umoja wa Mataifa, 14 Oktoba 2006, S/RES/1718 (2006), linalopatikana hapo: <https://undocs.org/S/RES/1718(2006)>

[3] *Azimio la Baraza la Usalama la 1874 (2009)*, 12 Juni 2009, S/RES/1874 (2009), linalopatikana hapo: <https://undocs.org/S/RES/1874(2009)>; *Azimio la Baraza la Usalama la 2087 (2013)*, 22 Januari 2013, S/RES/2087 (2013), linalopatikana hapo: <https://www.undocs.org/S/RES/2087(2013)>; *Azimio la Baraza la Usalama la 2094 (2013)*, 7 Machi 2013, S/RES/2094 (2013), linalopatikana hapo: <https://undocs.org/S/RES/2094(2013)>; *Azimio la Baraza la Usalama la 2270 (2016)*, 2 Machi 2016, S/RES/2270 (2016), linalopatikana hapo: <https://undocs.org/S/RES/2270(2016)>; *Azimio la Baraza la Usalama la 2321 (2016)*, 30 Novemba 2016, S/RES/2321 (2016), linalopatikana hapo: <https://undocs.org/S/RES/2321(2016)>; *Azimio la Baraza la Usalama la 2371 (2017)*, 5 Agosti

Majukumu ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Vikwazo

Kwa ajili maazimio haya yaliidhinishwa na Baraza la Usalama chini ya Sura ya VII ya Katiba ya Umoja wa Mataifa,[4] mataifa yana jukumu la kisheria chini ya Katiba ya Umoja wa Mataifa la kuhakikisha utekelezaji kisheria na utekelezaji kikamilifu, ikiwemo kuidhinisha hati za kikatiba, kisheria na kikanuni ili kuwezesha haya.

Ili kurahisisha utekelezaji, serikali zinafaa kuidhinisha mfumo wa kutekeleza vikwazo wa serikali-nzima unaoongozwa na mratibu wa kitaifa na unaohusisha wahusika wote wa utekelezaji wa serikali na wasiokuwa wa serikali.

Hatua, Utekelezaji na Kuripoti

Hatua za vikwazo ndani ya mfumo wa vikwazo wa 1718 zinaweza kugawanywa kwa ain tatu:

1. Marufuku na makatazo;
2. Vizuizi vya miundombinu;
3. Kupinga shughuli za kidiplomasia na kitamaduni.

2. ***Marufuku na Makatazo***

Korea Kaskazini imewekewa marufuku na makatazo yafuatayo:

- Silaha za kawaida na vifaa vyenye matumizi mawili;
- Teknolojia za usambazaji, zikiwemo silaha za maangamizi makubwa (WMD), bidhaa zenye matumizi mawili zinazohusu usambazaji na matakwa ya Husisha-Zote;
- Bidhaa;
- Bidhaa za anasa;
- Ulanguzi wa binadamu na kufanyishwa kazi kwa kutishiwa.

Silaha za Kawaida

Korea Kaskazini ni nchi pekee inayolengwa na marufuku ya silaha za kawaida ya pande mbili, ambayo inamaanisha kuwa uuzaji nje hadi na uingizaji nchini kutoka Korea Kaskazini wa silaha na vifaa husika hauruhusiwi.

2017, S/RES/2371 (2017), linalopatikana hapo: <https://undocs.org/S/RES/2371(2017)>; *Azimio la Baraza la Usalama la 2375 (2017)*, 11 Septemba 2017, S/RES/2375 (2017), linalopatikana hapo: <https://undocs.org/S/RES/2375(2017)>; *Azimio la Baraza la Usalama la 2397 (2017)*, 22 Disemba 2017, S/RES/2397 (2017), linalopatikana hapo: <https://undocs.org/S/RES/2397(2017)>

[4] *Katiba ya Umoja wa Mataifa*, Umoja wa Mataifa, 26 Juni 1945, inayopatikana hapo: <https://www.un.org/en/sections/un-charter/chapter-vii/index.html> [Ch. VII]

Ili kung'amua ni bidhaa zinazohusishwa kwenye marufuku, serikali zinafaa kushauri orodha husika zinazodumishwa na Kamati ya 1718 kuhusiana na:

- bidhaa, nyenzo, zana, vifaa na teknolojia zinazohusu silaha za kawaida (S/2017/829);[5]
- bidhaa zenye matumizi mawili (S/2017/760). [6]

Utekelezaji sheria

Ni lazima serikali zichukue hatua zinazohitajika ili:

- kuzuia ufikishaji wa moja kwa moja au kivingine, uuzaji au uhamishaji wa silah hadi Korea Kaskazini, ardhi iliyoko kwenye mipaka yake, au raia au mashirika yake;
- kuzuia usafirishaji wa silaha hadi Korea Kaskazini kutoka au kupitia ardhi iliyoko kwenye mipaka yao;
- kuzuia usafirishaji wasilaha hadi Korea Kaskazini unaofanywa na raia wake au kwa kutumia ndege na vyombo vya maji vyenye bendera yake nchi hiyo;
- kukamata au kusajili silaha zinazotambuliwa kuwa zinakiuka marufuku;
- kuangamiza au kivingine kuzifanya zisiweze kutumika, au kuzihifadhi, au kuzihamisha hadi nchi nyingine ili zitupwe, silaha zozote zinazokamatwa (ikiwa imeidhinishwa na azimio husika).

Majukumu ya Kuripoti

Ni lazima serikali ziripoti hatua za utekelezaji na mikakati madhubuti, na pia ukiukaji na mazingatio, kuhusiana na:

- marufuku dhidi ya uingizaji nchini Korea Kaskazini wa silaha au bidhaa husika, zikiwemo bidhaa zenye matumizi mawili;
- marufuku dhidi ya uuzaji nje wa silaha na bidhaa husika kutoka Korea Kaskazini, yakiwemo uondoaji wowote wa wajibu.

Teknolojia za Usambazaji

Kama vile kwenye silaha za kawaida, Korea Kaskazini pia imewekewa marufuku ya usambazaji ya pande mbili inayokataza uingizaji nchini na uuzaji nje hadi Korea Kaskazini wa vijenzi vyovyote vinavyoweza kutumika kuunda au kudumisha mkusanyiko wa silaha za maangamizi makubwa.

---

[5] *Ripoti ya Kamati ya Baraza la Usalama iliyoanzishwa kwa kutii azimio la 1718 (2017) iliyotayarishwa kulingana na paragrafu ya 5 ya azimio la 2375 (2017)*, Umoja wa Mataifa, 2 Oktoba 2017, S/2017/829, inayopatikana hapo: <https://undocs.org/S/2017/829>

[6] *Ripoti ya Kamati ya Baraza la Usalama iliyoanzishwa kwa kutii azimio la 1718 (2006) iliyotayarishwa kulingana na paragrafu ya 5 ya azimio la 2371 (2017)*, Umoja wa Mataifa, 5 Septemba 2017, S/2017/760, inayopatikana hapo: <https://undocs.org/S/2017/760>

Ili kung'amua ni bidhaa zinazohusishwa kwenye marufuku, serikali zinafaa kushauri orodha husika zinazodumishwa na Kamati ya 1718 kuhusiana na:

- Bidhaa, nyenzo, zana, vifaa na teknolojia zinazohusu silaha za maangamizi makubwa (S/2017/728);[7]
- Bidhaa, nyenzo, zana, vifaa na teknolojia zinazohusu silaha za maangamizi makubwa zenye matumizi mawili (S/2017/822).[8]

Kwa ajili ya ukali mahususi wa mfumo wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa, mbali na zana za usamabazaji na ulinzi, bidhaa yoyote inaweza kuhusishwa kwenye marufuku chini ya matakwa ya husisha zote iwapo inachangia kwenye yoyote kati ya yafuatayo kuhusiana na Korea Kaskazini:

- Uwezo wa kijeshi;
- Uundaji wa Silaha za Maangamizi Makubwa zikiwemo vijenzi vya silaha za nyuklia, bayolojia na kemikali;
- Uundaji wa makombora ya mbali.

Utekelezaji sheria

Ni lazima serikali zichukue hatua zinazohitajika ili:

- kuzuia aina yoyote ya ufikishaji wa bidhaa zinazohusu usambazaji zilizoorodheshwa chini ya orodha zilizorejelewa hapo juu ili zisiingie nchini Korea Kaskazini;
- kuzuia bidhaa yoyote ambayo inaweza kuhusishwa kwenye matakwa ya Husisha-Zote isiingie nchini Korea Kaskazini, na kunapokuwa na shauku, wauzaji nje wanafaa kushauriana na mamlaka zao za kitaifa za kudhibiti biashara.

Majukumu ya Kuripoti

Ni lazima serikali ziripoti hatua za utekelezaji na mikakati madhubuti, na pia ukiukaji na mazingatio, kuhusiana na:

- marufuku yaliyowekewa vitu, mali, vifaa, bidhaa na teknolojia zinazoweza kuchangia kwa miradi yanayohusu, nyuklia, makombora ya mbali au miradi mengine ya silaha za maangamizi makubwa, zikiwemo vitu vyovyote vyenye matumizi-mawili, au vifaa vinavyohusishwa kwenye Matakwa ya Husisha-zote.

<u>Bidhaa</u>

---

[7] *Ripoti ya Kamati ya Baraza la Usalama iliyoanzishwa kwa kutii azimio la 1718 (2006) iliyotayarishwa kulingana na paragrafu ya 4 ya azimio la 2371 (2017)*, Umoja wa Mataifa, 22 Agosti 2017, S/2017/728, inayopatikana hapo: <https://undocs.org/S/2017/728>

[8] *Ripoti ya Kamati ya Baraza la Usalama iliyoanzishwa kwa kutii azimio la 1718 (2006) iliyotayarishwa kulingana na paragrafu ya 4 ya azimio la 2375 (2017)*, Umoja wa Mataifa, 29 Septemba 2017, S/2017/822, inayopatikana hapo: <https://undocs.org/S/2017/822>

Serikali zinafaa kujua kuwa bidhaa zisizoruhusiwa na zile zenye vizuizi maalum chini ya mfumo wa 1718.[9] Kwa ajili Korea Kaskazini na mashirikisho yake wanajulikana sana kwa juhudi zao za kukwepa vikwazo, ni wajibu wa serikali kudumisha sera ya kujua asili, wamiliki na wanunuzi wa bidhaa kupitia nyaraka, vyeti vya biashara na uangalifu unaoeleweka.

Utekelezaji sheria

Ni lazima serikali zichukue hatua zinazohitajika ili:

- kuzuia ununuzi wa bidhaa zilizobainishwa zinazotoka au zinazoelekea Korea Kaskazini, kwa raia na mashirika yake.

Majukumu ya Kuripoti

Ni lazima serikali ziripoti hatua za utekelezaji na mikakati madhubuti, na pia ukiukaji na mazingatio, kuhusiana na:

- juhudi zote za kuizuia Korea Kaskazini isiweze kufikisha, kuuza wala kusafirisha makaa ya mawe, chuma, mawe yenye madini ya chuma, dhahabu, mawe yenye madini ya titaniamu, mawe yenye madini ya vanadiamu, madini adimu ya ardhi, shaba, nikeli, fedha, risasi na mawe yenye madini ya risasi, chakula na bidhaa za ukulima (misimbo ya HS ya 12, 08, 07), mashine (msimbo wa HS wa 84), vifaa vya umeme (msimbo wa HS wa 85), ardhi na mawe yakiwemo magnesiti na magnesia (msimbo wa HS wa 25), kuni (msimbo wa HS wa 44), mafuta ya ndege, mafuta ya jeti ya aina ya naptha, mafuta ya jeti ya aina ya kerosini, mafuta ya roketi ya aina ya kerosini, vyombo vya usafiri (msimbo wa HS wa 89), mashine za viwanda au magari ya usafiri, vyakula vinavyotoka baharini, na nguo.
- ndani ya vipindi vya muda wa siku-90, akiba yoyote ya mafuta ghafi yanayoenda Korea Kaskazini na viwango maalum vya mafuta hayo;

Bidhaa za Anasa

Nchi pekee iliyowekewa vikwazo vya bidhaa za anasa ni Korea Kaskazini. Kiasili, mfumo wa 1718 unatoa fursa pana za ufasiri kwa serikali kuhusiana na yale yanayojumuisha bidhaa kama hizi.

Utekelezaji sheria

Ni lazima serikali zichukue hatua zinazohitajika ili:

- kuidhinisha ufafanuzi wa taifa wa bidhaa za anasa;[10]
- kuamua ni nani miongoni mwa watengenezaji, wauzaji wa jumla, madalali na wauzaji wake; wanaokidhi ufafanuzi huu na wanaofaa kujulishwa kuhusu vizuizi vinavyohusu Korea Kaskazini;

[9] *Mwongozo wa Utekelezaji* [ukurasa wa 42]

[10] Tazama, k.v., *Mwongozo wa Utekelezaji* [ukurasa wa 44]

- kutekeleza sheria ya katazo kwa hatua za utekelezaji kupitia mifumo ya kudhibati uuzaji nje kwa kushirikiana na mawakala ya kudhibiti mipaka na sekta za usafiri.

Majukumu ya Kuripoti

Ni lazima serikali ziripoti hatua za utekelezaji na mikakati madhubuti, na pia ukiukaji na mazingatio, kuhusiana na:

- juhudi yoyote ya kutekeleza marufuku yaliyowekewa bidhaa za anasa.

Ulanguzi wa Binadamu na Kufanyishwa Kazi kwa Kutishiwa

Kuna katazo la jumla dhidi ya kutoa vibali vya kufanya kazi kwa raia wa Korea Kaskazini wanaofanya kazi ng'ambo.

Utekelezaji sheria

Ni lazima serikali zichukue hatua zinazohitajika ili:

- kuzuia vibali vya kufanya kazi visipewe raia wa Korea Kaskazini;
- kufukuza nchini watu wanaotambuliwa;
- kufukuza nchini wafanyakazi wa kibalozi na kidiplomasia walioteuliwa kama wasimamizi.

Majukumu ya Kuripoti

Ni lazima serikali ziripoti hatua za utekelezaji na mikakati madhubuti, na pia ukiukaji na mazingatio, kuhusiana na:

- kuwarudisha kwao wafanyakazi wote nchini wanaotoka Korea Kaskazini wanaolipwa;
- kuzuia kutumia vibaya ziara za kidiplomasia zinazotoa usaidizi au zinazoficha mradi wa usambazaji wa Korea Kaskazini, ikiwemo kufunga ziara za kidiplomasia au kufika nchini wafanyakazi wa kidiplomasia.

3. ***Vizuizi vya Miundombinu***

Korea Kaskazini imewekewa vizuizi vifuatavyo:

- ukwamishaji mali;
- kunyima huduma za fedha;
- katazo la usafiri;
- vizuizi vinavyowekewa usafiri wa baharini, ardhini na angani.

Ukwamishaji Mali

Ni lazima serikali zilazimu taasisi za fedha, zikiwemo sekta husiani kama vile mahasibu, maajenti wa nyumba, madalali wa fedha na hisa, maajenti wa bima, wafanyabiashara wa sarafu au washauri wa uwekezaji, wakwamishe mali yote yanayoweza kutambuliwa kwenye maelezo yanayotolewa kwenye orodha ya watu binafsi, kampuni au mashirika yaliyoorodheshwa kwenye 1718,[11] kulingana na viwango vilivyowekwa na kupendekezwa na Maafisa wa Kikazi wa

Matendo ya Kifedha (FATF).[12]

Utekelezaji sheria

Ni lazima serikali zichukue hatua zinazohitajika ili:

- kuzuia fedha au rasilimali zozote za kiuchumi ambazo tayari zinamilikiwa au kusimamiwa, moja kwa moja au kivingine, na mtu binafsi, kampuni au kundi lolote lingine lililoorodheshwa.
- kuzuia fedha au rasilimali zozote za kifedha zinazotolewa fursa zitumiwe na mtu binafsi, kampuni, au kundi lolote lingine lililoorodheshwa.
- kuzuia kampuni yoyote shiriki au husiani (mtu binafsi au shirika) inayofanya shughuli kwa niaba ya au kwa kufuata maagizo ya, au inayomilikiwa au kudhibitiwa na, watu binafsi, kampuni au mashirika ambayo tayari yameorodheshwa, ikiwemo vyombo vya baharini.

Majukumu ya Kuripoti

Ni lazima serikali ziripoti hatua za utekelezaji na mikakati madhubuti, na pia ukiukaji na mazingatio, kuhusiana na:

- juhudi zozote za kutekeleza ukwamishaji mali na katazo la usafiri; na pia mali yaliyokwamishwa, yakiwemo viwango maalum vya mali hayo na mahali zilipo,
- Hatua zinachukuliwa ili kufanya ukaguzi, ukwamishaji mali au tendo lingine linalofaa;

Kunyima Huduma za Fedha

[11] *Orodha iliyoanzishwa na kudumishwa kwa kutii azimio la Baraza la Usalama la 1718 (2006)*, Umoja wa Mataifa, inayopatikana hapo: <https://www.un.org/securitycouncil/sanctions/1718/materials>

[12] *Viwango vya Kimataifa vya Kupigana na Ulanguzi wa Fedha na Ufadhili wa Ugaidi na Usambazaji – Mapendekezo ya FATF*, Maafisa wa Kikazi wa

Matendo ya Kifedha, Oktoba 2018, vinvyopatikana hapo: <http://www.fatf-gafi.org/media/fatf/documents/recommendations/pdfs/FATF%20Recommendations%202012.pdf>

Ni lazima serikali zinyime huduma za fedha zinazounga mkono shughuli za usambazaji za Korea Kaskazini kwa kuhakikisha kuwa taasisi zao za fedha zinatekeleza uanagalifu unaoeleweka , kulingana na viwango vinavyopendekezwa na FATF.[13]

Utekelezaji sheria

Ni lazima serikali zichukue hatua zinazohitajika ili:

- kuzuia uhamisho wa mali au rasilimali zozote za fedha;
- kuzuia ufunguaji na uendeshaji wa matawi mapya, kampuni zinazomilikiwa au ofisi wakilishi za benki za Korea Kaskazini;
- kuzuia uendelezaji wa shughuli za matawi, kampuni zinazomilikiwa na ofisi wakilishi zilizoko, ushirikiano wa pamoja au maslahi ya umiliki, na uhusiano na benki za nje;
- kuzuia ufunguaji wa kampuni zinazomilikiwa na ofisi mpya za uwakilishi, matawi na akaunti za benki nchini Korea Kaskazini;
- kuzuia uendelezaji wa shughuli za akaunti za benki, kampuni zinazomilikiwa au ofisi zilizopo za uwakilishi nchini Korea Kaskazini;
- kuzuia usaidizi wa kifedha wa umma na kibinafsi wa biashara inayofanywa na Korea Kaskazini kama vile mikopo ya uuzaji nje, dhamana au bima;
- kuzuia kujitolea kupya kufikisha ufadhili, usaidizi wa kifedha, au mikopo ya ukabidhi nchini Korea Kaskazini.

Majukumu ya Kuripoti

Ni lazima serikali ziripoti hatua za utekelezaji na mikakati madhubuti, na pia ukiukaji na mazingatio, kuhusiana na:

- juhudi zozote za kuzuia ufikishaji wa huduma za miamala ya fedha, udalali au huduma zingine za mpito, wasafirishaji-pesa, huduma za bima au bima-upya za vyombo vya baharini, uondoaji wa fedha, mafunzo ya kiufundi, ushauri, huduma au usaidizi unaohusiana na ufikishaji, utengenezaji, udumishaji, au matumizi ya bidhaa zilizopigwa marufuku;
- uzuiaji wa miradi yote ya pamoja au shughuli za ushirikiano na watu binafsi au mashirika ya Korea Kaskazini.

Katazo la Usafiri

Chini ya mfumo wa 1718, ni lazima serikali zitekeleze kisheria katazo la usafiri dhidi ya:

- watu binafsi walioorodheshwa na orodha ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa;
- wanafamilia wao;
- wale wanaofanya matendo kwa niaba ya watu walioorodheshwa;

[13] *Viwango vya Kimataifa vya Kupigana na Ulanguzi wa Fedha na Ufadhili wa Ugaidi na Usambazaji – Mapendekezo ya FATF*, Maafisa wa Kikazi wa

Matendo ya Kifedha, Oktoba 2018, vinvyopatikana hapo: <http://www.fatf-gafi.org/media/fatf/documents/recommendations/pdfs/FATF%20Recommendations%202012.pdf>

- watu wowote ambao nchi imetambua kuwa wanafanya shughuli kwa niaba ya watu wanaosaidia ukwepaji wa vikwazo au wanaokiuka matakwa ya maazimio ya vikwazo vilivyowekewa Korea Kaskazini.

Utekelezaji sheria

Ni lazima serikali zichukue hatua zinazohitajika ili:

- kuzuia watu wowote waliorodheshwa kwenye orodha ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa, na pia wanafamilia wao na mtu yoyote binafsi anayefanya matendo kwa niaba yao au kwa kufuata maagizo yao asiingie wala asipitie nchi yao;
- kuzuia mtu yoyote binafsi ambaye nchi inaamua kuwa anakiuka matakwa ya maazimio ya vikwazo au anasaidia ukwepaji wa vikwazo asiingie wala asipitie nchi yao;
- kuzuia mtu yoyote anayesafiri kwa malengo ya kufanya shughuli zinazohusu usafirishaji wa bidhaa zisizoruhusiwa hadi au kutoka nchini Korea Kaskazini ili zifanyiwe urekebishaji, uhudumiaji, uundaji upya, upimaji, uhandisi-kinyume, na utafutaji soko siingie wala asipitie nchi yao;
- kufukuza nchini watu binafsi waliotajwa hapo juu.

Majukumu ya Kuripoti

Ni lazima serikali ziripoti hatua za utekelezaji na mikakati madhubuti, na pia ukiukaji na mazingatio, kuhusiana na:

- kuwarudisha kwao wafanyakazi wote nchini wanaotoka Korea Kaskazini wanaolipwa;
- kuzuia kutumia vibaya ziara za kidiplomasia zinazotoa usaidizi au zinazoficha mradi wa usambazaji wa Korea Kaskazini, ikiwemo kufunga ziara za kidiplomasia au kufika nchini wafanyakazi wa kidiplomasia.

Vizuizi vinavyowekewa Usafiri wa Baharini, Ardhini na Angani

Haki huria za Korea Kaskazini za kuzimamia kampuni na njia zake za usafiri ziko chini ya mamlaka ya vizuizi vipana.[14] Utekelezaji kisheria wa vizuizi hivi unavipatia majukumu vikosi vya wanamaji vya serikali, mamlaka za usafiri wa ndege na bahari, mamlaka za poti na udhibiti wa mipaka, mivuko ya barabara na treni, kampuni za bima ya meli, mawakala ya kuajiri na wamiliki wa meli.

Utekelezaji sheria

Ni lazima serikali zichukue hatua zinazohitajika ili:

- kuzuia vyombo vya usafiri vilivyoorodheshwa visiweze kupokea:
    - haki ya kupakia, kusafirisha, au kumwaga bidhaa za mafuta ya petroli;
    - ruhusa ya kuingia kwenye poti;
    - huduma za uegeshaji;

[14] *Mwongozo wa Utekelezaji* [kurasa za 52-54]

- miamala ya fedha ya ufikishaji wa petroli.

Majukumu ya Kuripoti

Ni lazima serikali ziripoti hatua za utekelezaji na mikakati madhubuti, na pia ukiukaji na mazingatio, kuhusiana na:

- juhudi zozote za kuondoa usajilini vyombo vinavyoshukiwa kuwa vinasafirisha bidhaa zilizopigwa marufuku;
- ukaguzi, ukamataji na utupaji wa bidhaa zinazorejeshwa wakati wa ukaguzi wa mizigo kwenye maeneo yao na ndani ya vyombo vilivyoko baharini;
- kutoshirikiana kwa nchi ya bendera ambapo chombo kinaaminiwa kuwa kinasafirisha bidhaa zilizowekewa marufuku;
- maelezo kuhusu usafirishaji, kubadilisha jina au kusajili upya;
- maelezo kuhusu idadi, jina na usajili wa vyombo vilivyoorodheswa vinavyopatikana kwenye eneo lake au baharini;

4. ***<u>Kupinga Shughuli za Kidiplomasia na Kitamaduni</u>***

   Kategoria hii ya vikwazo inajumuisha hatua zifuatazo:
   - Kuzuia hadhi za kidiplomasia;
   - Kuzuia biashara ya bidhaa za kitamaduni;
   - Kuzuia huduma za elimu;
   - Kuzuia shughuli za michezo;

<u>Kuzuia Hadhi za Kidiplomasia</u>

Kwa sasa hakuna vikwazo vilivyowekewa hadhi za kidiplomasia za Korea Kaskazini. Hata hivyo, watu binafsi wenye hadhi ya kidiplomasia bado wanaweza kuwekewa vikwazo vingine, ikiwemo makatazo ya usafiri na ukwamishaji mali, na wanaweza kukatazwa kuingia nchini na kwa hivyo, kufukuzwa nchini.

<u>Kuzuia Biashara ya Bidhaa za Kitamaduni</u>

Kwa ajili biashara ya bidhaa za kisanaa na kitamaduni ni chanzo muhimu cha mapato cha Korea Kaskazini, haswa barani Afrika,[15] mfumo wa 1718 unaidhinisha katazo la biashara hii.

Utekelezaji sheria

Ni lazima serikali zichukue hatua zinazohitajika ili:

[15] *Mwongozo wa Utekelezaji* [kurasa za 15-16]

- kuzuia ufikishaji, uuzaji na uhamishaji wa masanamu unaofanywa na mashirika na raia wa Korea Kaskazini.

Majukumu ya Kuripoti

Ni lazima serikali ziripoti hatua za utekelezaji na mikakati madhubuti, na pia ukiukaji na mazingatio, kuhusiana na:

- juhudi zote za kuizuia Korea Kaskazini isiweze kufikisha, kuuza au kuhamisha masanamu ya kisanaa.

Kuzuia Huduma za Elimu

Kwenye mfumo wa 1718, raia wa Korea Kaskazini hawaruhusiwi kupokea mafunzo au elimu inayoweza kuchangia kwenye usambazaji na uundaji wa makombora ya mbali, na pia hawaruhusiwi kupoka elimu na mafunzo ya jumla ya kijeshi kwa mujibu wa marufuku ya silaha.

Utekelezaji sheria

Ni lazima serikali zichukue hatua zinazohitajika ili:

- kuzuia raia au mashirika ya Korea Kaskazini yasiweze kufaidika na huduma za elimu kuhusiana na sayansi za usambazaji, zikiwemo kozi za hali ya juu za sayansi ya nyenzo, uhandisi wa kemikali, uhandisi wa mitambo, uhandisi wa umeme na uhandisi wa viwanda, na mafunzo yoyote mengine yanayohitajika ili kuunda teknolojia za silaha za nyuklia na makombora ya mbali;
- kuzuia ufikishaji wa aina yoyote ya mafunzo ya kijeshi ay ushauri wa kiufundi kwa raia au mashirika ya Korea Kaskazini.

Majukumu ya Kuripoti

Ni lazima serikali ziripoti hatua za utekelezaji na mikakati madhubuti, na pia ukiukaji na mazingatio, kuhusiana na:

- kuzuia mafunzo au elimu ya maalum, au ushirikiano wa sayansi na ufundi unaoweza kuusaidia mradi wa usambazaji wa Korea Kaskazini.

Kuzuia Shughuli za Michezo

Ingawa hakuna vikwazo vya shughuli za michezo vilivyowekewa Korea Kaskazini, katazo la bidhaa za anasa lina athari isiyo ya moja kwa moja kwenye shughuli kama hizi kwa ajili vifaa vya michezo mara nyingi huwa vinachukuliwa kuwa ni bidhaa za anasa.

5. Kuondolea wajibu

Kama kamati zote za vikwazo, Kamati ya 1718 ina mfumo wake wenyewe wa kupokea na kuidhinisha kuondolea wajibu, ikiwemo violezo na taratibu maalum.[16] Kuondolea wajibu kunafaa kuzingatiwa na Kamati ya 1718 kulingana na hali, chini ya mamlaka ya notisi ya mapema, na kuondolea wajibu kunaweza kuondolewa kwa sababu yoyote. Inapokuwa inaruhusiwa na azimio husika, ni lazima serikali ziwasilishe ombi la kuondolea wajibu mapema kwa kuarifu Kamati, huku ni lazima wahusika wasiokuwa wa serikali wawasilishe ombi kupitia ziara ya kudumu ya nchi ambao wao ni wakaazi/wamesajiliwa.

Kuondolea Wajibu wa Marufuku ya Silaha za Kawaida

Kuhusiana na marufuku ya silaha za kawaida, kuondolea wajibu kwa jumla huwa kunapewa kwenye hali ambapo inahakikisha uendeshaji salama wa ziara za Umoja wa Mataifa au ziara zingine za kudumisha amani na wawakilishi wa vyombo vya habari vya kimataifa na mashirika yasiyokuwa ya serikali. Ni lazima ombi la kuondolewa wajibu linalofanikiwa liorodheshe:

- Asili na idadi halisi ya bidhaa na huduma zote ambazo zinatakiwa ziondolewe wajibu;
- Mfululizo wa umiliki wa bidhaa au huduma kwenye kipindi cha muda ambapo zitatumiwa ndani ya eneo lililowekewa marufuku;
- Mamlaka na idhini ambazo zinatumiwa kufikisha vitu hivi kwenye eneo lililowekewa marufuku;
- Shirika lenye jukumu la usafirishaji wa bidhaa zilizopigwa marufuku;
- Poti ya kuingia.

Kuondolea Wajibu wa Makatazo ya Usafiri na Ukwamishaji Mali

Kuondolea Wajibu wa Makatazo ya Usafiri na Ukwamishaji Mali kunaweza kukubaliwa:

- kwa misingi ya kibinadamu, ikiwemo kufikia huduma za kimatibabu au kutimiza majukumu ya kidini;
- ili kurahisisha kushiriki kwenye taratibu za upatanishi na mazungumzo;
- kwa sababu zingine.

Kuondolea wajibu huwa kwa asili yake ni wa kipekee na kunafanyika tu kwenye hali ambapo kufanya hivyo hakutovunja mfumo wa 1718.

***

[16] *Mwongozo wa Utekelezaji* [kurasa za 80-83]

Mark Duncan

Mark Duncan ni mwanafunzi aliyehitimu na mtafiti mwenye uzoefu mwingi kwenye upokonyaji silaha, kupinga usambazaji, na udhibiti wa silaha. Kwa sasa yeye ni mkufunzi kwenye Ziara ya Kudumu ya Afghanistani kwenye Umoja wa Mataifa. Hapo awali, alikuwa mkufunzi kwenye Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Masuala ya Upokonyaji Silaha, Baraza la Masuala ya Kimataifa la Urusi na Kituo cha Kimataifa cha Kuchambua Usalama. Alihitimu kutoka UCL na Shule Kuu ya Uchumi, Mosko na Shahada ya Uzamili ya Kimataifa ya Uchumi, Nchi, na Jamii: Amani na Usalama Atajiunga na Ofisi ya Jumuiya ya Madola na Mambo ya Nje kama Mtiririshaji Upesi wa Huduma za Kiraia mbeleni mwaka huu.